AJIRA

# Ulega: Vijana changamkieni fursa za uchumi wa buluu

Mwandishi Wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Mwanza.** Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amewahimiza vijana wa kanda ya ziwa kufuga samaki ili kujiongezea kipato na kuongeza fursa za ajira nchini.

Ulega alitoa wito huo mwishoni mwa wiki akiwa ziarani katika wilaya za Ukerewe na Ilemela zilizopo mkoani Mwanza.

Alisema Serikali imejipanga kutumia fursa za uchumi wa buluu zilizopo ndani ya Ziwa Viktoria kuwawezesha vijana kufuga samaki kwa kutumia vizimba na kuwauza samaki hao ndani na nje ya nchi ili kujiongezea kipato.

"Rais Samia Suluhu Hassan ametoa Sh20 bilioni kwa ajili ya kuwawezesha vijana kufuga samaki katika vizimba, hivyo ni wakati sasa wa kujipanga ili pesa hizo zitakapokuja tuweze kuzitumia vizuri kufanya uzalishaji wa samaki kwa wingi ili tuweze kuuza na kupata kipato," alisema Ulega.

Alisema samaki aina ya sato wanahitajika sana ndani na nje ya nchi hivyo vijana wajipange vizuri ili waweze kuitumia fursa hiyo kujiinua kimaisha kwa kushiriki kwenye ufugaji.





> 'Mwaka huu Serikali itawakopesha wavuvi nchini kote boti za kisasa zaidi ya 150 ili wavuvi waboreshe shughuli zao na kuongeza uzalishaji wa samaki.'
>
> **Abdallah Ulega, naibu waziri**

Kwa upande wake, mfugaji wa samaki, Bahati Paul kutoka Ilemela alisema mpango huo wa Serikali wa kuwawezesha vijana utasaidia kuongeza ajira na wakaiomba

"Kuna changamoto ya upatikanaji wa chakula cha samaki. Bei yake ni kubwa na inatuongezea wafugaji gharama za uendeshaji wa miradi hii, naiomba Serikali isaidie kuitatua changamoto hii," alisema Paul.

Katika hatua nyingine, Waziri Ulega alisema mwaka huu Serikali itawakopesha wavuvi nchini kote boti za kisasa zaidi ya 150 ili wavuvi waboreshe shughuli zao na kuongeza uzalishaji wa samaki kukidhi mahitaji nchini hata kwenye mikoa isiyovua ili kuongeza ulaji wa kitoweo hicho.

Aliongeza kuwa boti hizo zitafungamanishwa na teknolojia ya kisasa itakayomsaidia mvuvi kurahisisha shughuli zake hivyo kupata kiasikingi kitakachoongeza kipato chake.

Waziri Ulega alifafanua kuwa mkopo huo wa masharti nafuu unalenga kuwawezesha wavuvi kuboresha uvuvi kwa sababu nia ya Rais Samia ni kuwatoa katika uvuvi wa kuwinda na kufanya uvuvi wa kisasa wenye uhakika wa kupata samaki wawatakao.

Scanned with CamScanner

CamScanner

HABARI LEO UK 12.



Mtaalamu wa kufuga samaki katika Shamba la Samaki la Son Fish Farm, la nchini Uganda, Joseph Nsenga (kulia) akitoa elimu kwa Watanzania waliotembelea shamba hilo kwa mafunzo hivi karibuni.



Mtafiti wa Afya ya Viumbe wa Majini kutoka Taasisi ya NAFIRRI, Uganda, Cathe[illegible] Agoe (kushoto), akiwaonesha Watanzania waliofanya ziara ya mafunzo nchini hu[illegible] dawa za maradhi ya samaki zilizotengenezwa kwa mimea asili hivi karibuni.

# Madoa, kuogelea tumbo juu dalili ya samaki mgonjwa

Na Abel [illegible]sikula

SAMAKI wa kufugwa akiogelea wakati wote juu ya maji au kuzama chini kabisa, huyo ni mgonjwa. Anapoogelea mgongo chini tumbo juu, akawa na kona nyingi kwenye maji zisizo na mwelekeo maalumu pia ni dalili ya kuumwa.

Halikadhalika anapopewa chakula akashindwa kukishambulia, mfugaji atambue kwamba samaki wake huyo anaumwa.

"Au samaki anaweza kuwa na alama nyingi zenye sura ya vidonda au madoa ya rangi nyekundu au nyeusi mwilini. Huo pia ni ugonjwa," anasema mtaalamu wa kufuga samaki katika Shamba la Samaki lijulikanalo Son Fish Farm lililopo Jinja nchini Uganda, Joseph Nsenga.

Anasema maradhi yanayoshambulia samaki kwa wingi ni fangasi, ambao husababisha ngozi ya samaki pamoja na masikio kuoza au kuwa na mabaka.

Alitoa elimu hiyo wiki iliyopita nchini Uganda wakati wa ziara ya mafunzo na wafugaji samaki kwa njia ya vizimba wa Wilaya ya Ilemela, mkoani Mwanza, Tanzania, iliyoratibiwa na Ubalozi wa Tanzania nchini Uganda kwa kushirikiana na Shirika la Samaki Ziwa Victoria (LVFO).

Nsenga anasema kwa sasa dawa inayotumika kwa maradhi ya fangasi kwa samaki ni chumvi, ambapo kama ufugaji unafanyika kwenye madimbwi mfugaji anapaswa kufungulia maji yapungue na kubaki robo, kisha amimine chumvi.

Anasema hilo linaweza kufanyika kwa siku tano hadi wiki moja itakuwa tayari ngozi ya samaki itakuwa imerudi katika hali yake ya kawaida.

"Na muelekeo wa kuogelea pia utakuwa sawa, kwani kawaida samaki huogelea mgongo ukiwa juu na muelekeo wake unakuwa unenyooka, bila kona yoyote," anasema.

Hata hivyo, watafiti nchini humo, ikiwemo Kituo cha Utafiti wa Viumbe Maji Kajjansi cha Taasisi ya Utafiti wa Rasilimali za Uvuvi nchini Uganda (NAFIRRI) jijini Kampala wanapambana kupata dawa za maradhi ya samaki.

Mtafiti wa afya ya viumbe wa majini, Catherine Agoe, anasema kituo hicho kimejikita zaidi kwenye utafiti wa dawa za asili ili kuepuka matumizi ya dawa za viwandani ambazo zinaweza kupoteza ubora wa samaki na huenda zikaleta madhara mengine katika maji na kwa viumbe wenyewe.

Hadi sasa kituo kimefanikiwa kutengeneza dawa za miti shamba na kuzisambaza maduka ya dawa kadhaa nchini humo, huku mahitaji ukiendelea kuwa makubwa.

Dawa hizo ni kwa magonjwa hasa ya bakteria, fangasi, vimelea pamoja na virusi, anasema na kuwasisitiza wafugaji kupata tiba mapema kwani



Mtafiti Mwandamizi wa Taasisi ya NAFIRRI, Uganda, Dk Margaret Aanyu (kulia), akitoa elimu ya ufugaji samaki kwa Watanzania waliofanya ziara ya mafunzo nchini humo hivi karibuni.

virusi na bakteria ni maradhi yanayoua samaki haraka.

"Ili kuzuia magonjwa ya samaki, tunashauri wafugaji kuchagua sehemu sahihi ya kufugia, ikiwemo kufahamu kwanza eneo hilo lilikuwa na matumizi gani kabla ya kujenga miundombinu ya kufugia samaki," anasema Agoe.

Vilevile anasema mfugaji ahakikishe chanzo cha maji yatakayotumika kwa ufugaji hayana aina yoyote ya uchafu au sumu na wingi wa samaki uzingatie ukubwa wa dimbwi au kizimba ili kuepuka msongamano wa viumbe hao.

Anasema msongamano ukiwa mkubwa samaki watakosa hewa ya kutosha, watadumaa, watapata msongo pamoja na msuguano wakati wa kugombea eneo au chakula.

Kugombania kunawasababishia michubuko na hivyo kuwa chanzo cha magonjwa kwa samaki hao.

Agoe anamshauri mfugaji ahakikishe ubora wa maji yanayotumika kufugia unakidhi viwango kwa maana ya kuwa na hewa ya Oksijeni pamoja na joto linalohitajika.

Dimbwi au kizimba kiwekewe miundombinu yenye ulinzi, hasa vyavu, ili kuwalinda na adui ambao mara nyingi huwajeruhi samaki na hatimaye majeraha hayo kuwa chanzo cha magonjwa.

"Mfugaji ahakikishe asilimia takribani 25 ya maji kwenye dimbwi inaondolewa na kujaza maji mapya angalau kwa mwezi mara moja," anasisitiza na kuongeza:

Mfugaji asiwape samaki chakula kingi zaidi ya uhitaji kwa sababu kinachobakia kitazama chini ya maji na kuoza, hivyo kuharibu ubora wa maji na hatimaye kuathiri samaki kwa namna mbalimbali.

Chakula cha samaki kitumike ndani au chini ya miezi miwili baada ya kutengenezwa na vilevile mfugaji ahakikishe hakuna mwingiliano wa samaki kutoka nje ya kizimba, kwa kuziba mitobo yote ya maji au kufunga nyavu vizuri.

Samaki kuto[illegible] za kuwa wak[illegible] kuwashambuli[illegible] wanaweza kup[illegible] na kuwaambukiza [illegible]

Kwenye [illegible] vifaranga wa sama[illegible] lilopo hewa [illegible] ya kuna vipindi [illegible] anayetika hapo [illegible] nyayo zake kuw[illegible] ka unaendelea [illegible] viumbe hao.

"Lakini pia [illegible] ahakikishe anaan[illegible] kutoka kwa w[illegible] waliothibitish[illegible] zote anapoa[illegible] asaki ahakikishe an[illegible] stahiki mak[illegible]" [illegible] Agoe.

Mtafiti M[illegible] Kituo hicho, Dk M[illegible] Aanyu, anasi[illegible] kwamba [illegible] kuweka dawa [illegible] mfugaji [illegible] maki [illegible] kwenye [illegible] ya kambe [illegible] nafisha baada [illegible] wanyo [illegible]

Kwa [illegible] viumbe [illegible] ngoma [illegible] atanuma [illegible] wakila [illegible] wadhuriki [illegible] maringira kup[illegible] Dk Aanyu.

Anasisitiza [illegible] dawa za asili [illegible] hazo tayari [illegible] mkubwa, ili k[illegible] viumbe hao [illegible] usalama wa [illegible]

Baada ya k[illegible] juu ya manfo[illegible] ufugaji samaki, [illegible] zania nchini Uganda [illegible] Mlima, aka[illegible] wa kituo hicho k[illegible] Tanzania ili k[illegible] fugaji wengi [illegible] mmoja.

Wataalamu [illegible] atayari waa[illegible] ili mradi wap[illegible] rasmi.

CS Scanned with CamScanner

CS CamScanner

HABARI LEO UK 4.

# Tanzania, Oman kuongeza ushirikiano maeneo ya uwekezaji, elimu na uvuvi

Na Mwandishi Wetu

TANZANIA na Oman zimeahidi kuongeza maeneo ya ushirikiano katika sekta za uwekezaji, elimu, uvuvi na utamaduni.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula alisema hayo alipokutana na kuzungumza na Balozi wa Oman nchini, Saudi Hilal Al Sidhani katika Ofisi Ndogo za Wizara jijini Dar es Salaam.

Taarifa ya wizara hiyo kwa vyombo vya habari ilieleza kuwa Balozi Mulamula alisema ni wakati sasa kwa mataifa hayo kuongeza ushirikiano katika sekta za uwekezaji, elimu, uvuvi na utamaduni kwa maendeleo ya mataifa yote.

Balozi wa Oman nchini, Al Sidhani alisema Oman ipo tayari kuwekeza katika maeneo yenye fursa hapa Tanzania.

"Naomba endapo Tanzania mtaona maeneo mapya ya ushirikiano hususani fursa za uwekezaji na biashara msisite kutushirikisha tukajadiliana na kuitekeleza azma hiyo kwa maslahi ya pande zote mbili," alisema Balozi Al Sidhani.

Wakati huohuo, Balozi Mulamula amepongeza jitihada za Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Ukimwi (UNAIDS) hasa kutoa elimu na kampeni dhidi ya Maambukizi ya Virusi vya Ukimwi.

Alitoa pongezi hizo katika Ofisi Ndogo za Wizara Dar es Salaam baada ya kupokea barua za utambulisho za Mkurugenzi Mkazi wa UNAIDS, Martin Odiit.

Balozi Mulamula alimhakikishia Odiit ushirikiano wa serikali wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yake nchini na akasema UNAIDS imesaidia kupunguza maambukizi ya Ukimwi kwenye jamii.

Odiit alisema UNAIDS itaendelea kuelimisha jamii ya Kitanzania na kuhakikisha hadi mwaka 2025 maambukizi ya Virusi vya Ukimwi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto atakayezaliwa yatakuwa yamepungua kwa asilimia 95.

Scanned with CamScanner

CamScanner